# Uponyaji Kutokana na Talaka

Hapo mwanzo, Mungu alimuumba Adamu na Hawa na akakusudia waunganishwe kama mume na mke: *"Ndiyo maana mwanamume humwacha baba yake an mama yake, akaambatana na mkewe, nao wawili huwa mwili mmoja.* " (Mwanzo 2:24; vilevile Marko 10:6-9). Paulo anaeleza kwamba kusudi la Mungu katika uhusiano wa ndo katia ya mume na mke linaweza kutumiwa kama picha ya kusudi la Mungu la uusiano kati ya Yesu na kanisa lake (Waefeso 5:23). Zaidi ya hayo, Mungu aliwapa wanadamu hiari; kisha Shetani akaingilia kati na tangu wakati huo amekuwa akifanya kazi ya kuumaliza mpango wa Mungu katika uhusiano wa ndoa.

## Masuala Zaidi na Mambo ya Kusikitisha

1. Ndoa ni agano la kiroho kati ya Mungu na wanandoa na ni jambo muhimu sana kwa Mungu. Mungu alikusudia kuwe na aina moja tu ya ndoa (Mwa. 2:24, Mark0 10:6-9). Muungano wa nafsi wa kiungu huundwa kupitai kwa agano la ndoa.
2. Talaka haikua katika mpango wa Mungu wa kwanza, kwa hivyo, Yeye anaiona kuwa dhambi. Sheria za kiroho hukiukwa katika kitendo cha talaka (Mat. 5:32).
3. Kuna mambo hali tatu za kuthibitisha talaka zinazoweza kutambuliwa katika maandiko: (1) uzinzi (Mat. 5:32), (2) mwanandoa asiye Mkristo anapomwacha mwenzake (1 Kor. 7:15) au mwanandoa ambaye mwenzake amezini lakini yeye hajafanya dhambi kwa kumpa talaka mwenzake ana uhuru wa kuoa/kuolewa tana bila kutenda dhambi (Mat. 5:32), na (3) ingawaje kuiacha ndoa au dhambi za ngono zilizofanywa na mwenzi mmoja ni thibitisho halisi la talaka, vifungu vingine (kama vile 1 Kor. 7:2-5) vinapendekeza kwamba mwanandoa hayuko chini ya kifungo cha kuendelea kuwa katika ndoa na mtu anayevunja nadhiri ya **kumfanyia mtu wema unaostahili.**
4. Suala lenyewe—kimaandiko—si "sababu ya talaka" bali ni ikiwa mwanandoa atafanya mapenzi na mtu mwingine baada ya talaka, kwani maandiko yanakiita kitendo hicho uzinzi *("Anayempa mkewe talaka, isipokuwa kwa sababu ya uzinzi, anamfanya azini, na mwanamume akimwoa mwanamke aliyepewa talaka, anazini."*—Mat. 5:32).
5. Uzinzi unapofanyia, mpango wa Mungu wa "wawili huwa mwili mmoja" (Mwa. 2:24) hutatizwa, huchafuliwa, na kuvunjwa. Mpango huu unapovunjwa, hufungua mwanya wa nguvu za giza kupitia.
6. Mhubiri 5:4-6 inapendekeza kwamba laana ya talaka inaweza kumjia mtu kwa kuvunja nadhiri na Mungu (ndoa ni nadhiri).
7. Majeraha ya kukataliwa, hasira, na kuachwa yanaweza kudumu baada ya uhusiano kuvunjika.
8. Muungano wa nafsi huendelea kuweko kati ya wanandoa hao mpaka uvunjwe kiroho
9. Habari Njema ni kwamba, Mungu aliye mbinguni alimtuma Mwanawe Yesu Kristo kutufia msalabani ili tuweze **kusamehewa kila dhambi (**zikiwemo talaka, dhambi za ngono au uzinzi kwa kuoa/kuolewa tena), kuoshwa kwa damu ya Yesu, na kuwa na uhusiano mpya naye kwa nguvu za Roho Mtakatifu.
10. Jambo linalozingatiwa katika uponyaji kutokana na talaka si kutaka kujua ikiwa dhambi ilitendwa kupitia ka tukio hilo bali ni kuomba msamaha unaostahili na kukubali neema na msamaha wa Baba Yetu mwenye upendo.

## Kuombea Uponyaji Kutokana na Talaka

Mhusika anatakiwa kuzifuata hatua hizi:

1. Mwambie Mungu akusemehe kwa sehemu uliyochukua katika talaka (watu wote wawili hususika).
2. Mwambie Mungu akusamehe kwa dhambi zozote za ngono zilizotendeka kabla au baada ya talaka.
3. Mwambie Mungu akusamehe kwa ajili ya dhambi zolizosababishwa au kuoa/kuolewa tena.
4. Uponyaji kutokana na talaka unahitaji umsamehe kabisa mwenzi wako wa awali.
5. Omba kwamba sehemu yako iliyobaki na mwenzi wako itaachiliwa huru.
6. Omba ili upate uponyaji wa ndani kutuokana na hisia za kukataliwa, hasira au kuachwa.
7. Omba na kuvunja kwa upanga wa Roho, muungano wowote wa nafsi ulioletewa na muungano wa awali.
8. Iwapo mtu huyo hajaoa/hajaolewa, omba kwamba ataendelea kuishi peke yake ili asitende dhambi za ngono.
9. Iwapo mtu huyo ameoa/ameolewa tena, omba kwamba Mungu atautambua uhusiano huo wa sasa kama mpango wa asili uliopangwa mbinguni pamoja na haki zote na baraka za **agano la kupatana kwa wawili kuwa mwili mmoja.**
10. Omba ili Mungu abariki muungano huo na familia hiyo katika jina la Yesu..